

# Jinsi ya Kujiunga na Ziara yako ya Video ukiwa Nyumbani



## Jiandikishe Mtandaoni kupitia eCheck In:

Unaweza kujiandikisha kwa miadi yako ya mtandaoni, hadi siku saba kabla ya ziara yako au siku ya ziara.

1. Unapaswa kuwa umetumiwa barua pepe/ujumbe mfupi kutoka kwa Children's Mercy. Bofya kiungo. Ikiwa haipatikani, nenda kwenye MyChart na uchague "Find the eCheck" (Tafuta eCheck).



2. Ingiza tarehe ya kuzaliwa ya mgonjwa na ubofye "Verify" (Thibitisha).




3. Jiandikishe mtandaoni kwa kuingiza taarifa katika kila sehemu.

- o Mahali utakapokuwa wakati wa ziara ya video
- o Bima na taarifa ya malipo
- o Dawa ambazo mgonjwa hutumia
- o Duka la dawa unalotumia
- o Mizio yoyote ambayo mgonjwa anayo
- o Matatizo yoyote ya afya ambayo mgonjwa anayo
- o Maswali ya safari
- o Hojaji zozote ambazo daktari anahitaji

#### 4. Jaribu maikrofoni, kamera, spika na muunganisho wako.


- Kuwa mahali ambapo utatumia kifaa chako wakati wa ziara yako ya video.
- Bofya "Test hardware" (Jaribio la maunzi).



- Ukiombwa, ruhusu kamera na maikrofoni yako itumike.
- Tumia menyuaari kunjuzi kubadilisha kamera au maikrofoni yako ikiwa inahitajika.
- Tafuta alama za tiki za kijani zinazoonyesha kwamba majaribio yalifanikiwa. 🟢

#### 5. Bofya X ili kuondoka kwenye jaribio la maunzi mara tu linapokamilika.

#### 6. Bofya "Submit" (Wasilisha) kwenye eCheck In baada ya kukamilisha kila hatua.



#### 7. Kagua maelezo ya miadi kabla ya ziara yako ya video.


# Jinsi ya Kujiunga na Ziara yako ya Video ukiwa Nyumbani




## Kualika Watu Wengine kwenye Ziara yako ya Video:

Kiungo unachopokea katika ujumbe mfupi au barua pepe yako kinaweza kutumiwa na mtu mmoja pekee. Ikiwa watu wengine wanahitaji kujiunga na ziara hiyo, mwambie daktari mara tu ziara ikianza au uwaalike kabla ya ziara.


1. Nenda kwenye ukurasa wa maelezo ya miadi ya ziara yako ya video.
2. Ingiza tarehe ya kuzaliwa ya mgonjwa na ubofye "Verify" (Thibitisha).



3. Bofya "Invite a new guest" (Alika mgeni mpya).



4. Chagua mmoja wa wawasiliani wako waliopo ikiwa tayari wako kwenye mfumo.



**5. Bofya "Invite a new guest" (Alika mgeni mpya) na uweke taarifa yake ili kumwalika mtu ambaye hajaorodheshwa: "Test hardware" (Fanya jaribio la maunzi) ili kujaribu maikrofoni, kamera, spika na muunganisho wako wa intaneti.**

- o Jina la kwanza
- o Jina la Mwisho
- o Uhusiano na mgonjwa
- o Namba ya simu au anwani ya barua pepe ya kutuma mwaliko

**Guests**

Invite a guest to join this video visit, such as a family member or caregiver. Guests can join the video visit with the link in their invitation message. Guests may have been invited by your provider.

Select someone to invite:

Joe Smith Jane Doe + invite a new guest

\* Indicates a required field.

\* First name

\* Last name

\* Relationship

Text message  Email

\* Phone number

This person has agreed to receive a text message.

Send text message invitation Cancel

Text messages related to your relationship with Children's Mercy, including updates related to your visits, Children's Mercy MyChart account, one-time passcode, billing notifications, prescription reminders, and care management will be sent to phone number above. Message and data rates may apply. Message frequency may vary. For help text HELP and text STOP to opt out of notifications from a specific short code. Please review terms and conditions and privacy policy below.

[Terms and Conditions](#) [Privacy Policy](#)

**6. Bofya "Send text message" (Tuma ujumbe mfupi) au "Send email invitation" (Tuma mwaliko wa barua pepe).**

**7. Mgeni atapata arifa yenye kiungo cha kujiunga na ziara hiyo.**



# Jinsi ya Kujiunga na Ziara yako ya Video ukiwa Nyumbani




## Jiunge kwenye Ziara Yako ya Video

**1 Dakika 15 kabla ya ziara yako ya video, bofya kiungo cha ziara hiyo katika arifa ya barua pepe au ujumbe mfupi, au katika akaunti ya MyChart ya mgonjwa.**

- Usishiriki kiungo hicho na watu wengine. Mtu 1 pekee ndiye anayeweza kutumia kiungo hiki.
- Ikiwa watu wengine wanahitaji kujiunga na ziara hiyo, mwambie daktari mara tu ziara itakapoanza au uwaalike wengine kabla ya ziara.




**2 Jaribu maikrofoni, kamera, spika na muunganisho wako.**



- Ukiombwa, ruhusu kamera na maikrofoni yako itumike.
- Tumia menyu kunjuzi kubadilisha kamera au maikrofoni yako ikiwa inahitajika.
- Alama za tiki za kijani zinaonyesha kwamba sehemu ya jaribio ilifanikiwa. 
- Washa Manukuu ikiwa unataka kufanya hivyo. 
- Badilisha jina lako la kuonyesha ikiwa unataka kufanya hivyo. 

**3**Utawekwa kwenye chumba cha kusubiri cha mtandaoni. Daktari atajiunga na ziara hiyo baada ya kukagua taarifa yako.



**4**Usiondoke au kupunguza skrini ya ziara ya video hadi baada ya ziara yako kukamilika.


## Sasa kwa kuwa ziara imeanza:

- **Vitufe vya kudhibiti video viko kwenye kona ya juu, upande wa kulia wa ziara ya video.**




- **Connection Strength (Nguvu ya Munganisho):** 
  - Hii inaonyesha nguvu ya muunganisho wako wa intaneti. Unahitaji muunganisho thabiti ili kukamilisha ziara ya video au ziara yako itahitaji kupangwa upya.


- **More options (Machaguo zaidi):**




- **"Devices" (Vifaa)** hukuruhusu kubadilisha kamera, maikrofoni au spika zako
- **"Background effects" (Athari za mandharinyuma)** ndipo unapoweza kutia ukungu kwenye mandharinyuma yako.
- **"Full screen mode" (Halitumizi ya skrini nzima)** na "Switch to grid view" (Badilisha kwenda mwonekano wa gridi) hubadilisha muundo wa video.
- **"Language" (Lugha)** ina machaguo ya kubadilisha lugha ya machaguo ya maandishi katika ziara ya video.
- **"Show English captions" (Onyesha manukuu ya Kiingereza)** huwasha manukuu ya Kiingereza kwa ziara ya video.



- **Participants (Washiriki):** 
  - Tazama watu wote kwenye ziara ya video.
- **Camera and microphone (Kamera na maikrofoni):** 
  - Hakikisha kamera na maikrofoni yako imewashwa. Bofya kitufe ili uziwashe au uzizime.
- **Share screen (Shiriki skrini):** 
  - Shiriki kile kinachoonyeshwa kwenye skrini yako na daktari wako. Hii inaweza kutumika kuonyesha picha iliyohifadhiwa. Daktari ataweza kuona kila kitu kinachoonyeshwa kwenye skrini yako ukishiriki skrini yako.
- **Chat (Gumzo):** 
  - Unaweza kumtumia daktari wako ujumbe wakati wa ziara.
  - Bofya kitufe cha Chat (Gumzo) ili kufungua gumzo. Andika ujumbe wako kisha ubofye "Send" (Tuma).
  - Huwezi kuona gumzo baada ya ziara kukamilika.



- **Leave Call (Kata Simu):** 
  - Bofya "Leave call" (Kata simu) ili kumaliza ziara ya video.
  - Ikiwa unahitaji kujiunga tena na ziara baada ya kukata simu, bofya kiungo kwenye barua pepe yako au ujumbe mfupi na ujiunge na ziara hiyo tena.

## Changamoto za Kawaida na Masuluhisho


- **Nina matatizo ya kamera au maikrofoni.**

- Hakikisha kwamba kivinjari chako cha mtandao kinaruhusiwa kutumia maikrofoni na kamera yako.


- **Ikiwa unatumia kompyuta:**

- Mipangilio ya ruhusa ya Google Chrome:

1. Ukiwa kwenye ukurasa wa ziara ya video, bofya kitufe cha ruhusa au kamera kilicho upande wa kushoto wa upau wa kutafutia.



2. Hakikisha kwamba swichi za kamera, maikrofoni na sauti zimewashwa.




- Mipangilio ya ruhusa ya Microsoft Edge:

1. Ukiwa kwenye ukurasa wa ziara ya video, bofya kitufe cha kufunga kilicho upande wa kushoto wa upau wa kutafutia.



2. Hakikisha kwamba swichi za kamera na maikrofoni zimewashwa.




• **Ikiwa unatumia iPhone:**


- Hakikisha kwamba unatumia kivinjari cha mtandao cha Safari ikiwa unatumia iPhone.

1. Fungua mipangilio. 


2. Biringiza chini hadi kwenye Apps (Programu).



3. Bofya programu ya kivinjari cha mtandao unachotumia.




4. Bofya Camera (Kamera).



5. Hakikisha kwamba mipangilio imewekwa kuwa Ask (Uliza) au Allow (Ruhusu).

6. Rudi nyuma kisha ubofye Microphone (Maikrofoni).




7. Hakikisha kwamba mipangilio imewekwa kuwa Ask (Uliza) au Allow (Ruhusu).

• **Ikiwa unatumia simu ya Android:**


- Hakikisha kwamba unatumia kivinjari cha mtandao cha Chrome ikiwa unatumia simu ya Android.

1. Fungua mipangilio. 




2. Bingiriza chini kisha ubofye Apps (Programu) ili kufungua mipangilio ya programu.


3. Tafuta na ubofye programu ya kivinjari cha mtandao unachotumia.





4. Bofya Permissions (Ruhusa).



5. Menu hii inakuonyesha mambo ambayo yameruhusiwa na ambayo hayajapewa ruhusa.



- Ikiwa inaonyesha kwamba maikrofoni au kamera iko katika hali ya **Denied (Haijapewa ruhusa)**, bofya ili kuhariri mipangilio.
- Badilisha mpangilio ili kuruhusu kamera na maikrofoni itumike.



## Sipati kiungo cha ziara yangu

- **Kiungo hutumwa kwenye barua pepe na simu yako mara nyingi kabla ya ziara yako.**
  - Wakati wa kupanga.
  - Siku 7 kabla ya ziara.
  - Saa 24 kabla ya ziara.
  - Saa 1 kabla ya ziara.
  - Dakika 15 kabla ya ziara.
- **Usishiriki kiungo hiki na watu wengine. Mtu 1 pekee ndiye anayeweza kutumia kiungo hiki. Ikiwa watu wengine wanahitaji kujiunga na ziara hiyo, mwambie daktari mara tu ziara itakapoanza na uwatumie mwaliko kwenye ukurasa wa maelezo ya ziara.**
- **Hakikisha kwamba umeangalia folda zako za barua pepe Taka (Junk au Spam).**

**Kwa usaidizi kuhusu ziara yako ya video,  
piga simu kwa (816) 234-3000 na uchague chaguo la 5.  
Ili kupanga upya miadi yako, piga simu kwa (816) 234-3700**